Jinsi Ya Kubaki Mwaminifu Katika Bwana

Na

Ellis P. Forsman

(How To Remain Faithful To The Lord)

Jinsi Ya Kubaki Mwaminifu Katika Bwana.

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 12, 2011

Jinsi Ya Kubaki Mwaminifu Katika Bwana

Gal. 5:4

Gal. 5:4, "*Mmetengwa na Kristo, ninyi mtakao kuhesabiwa haki kwa sheria; mmeanguka na kutoka katika hali ya neema.*"

Inawezekana kwamba mara tunapokuwa washiriki wa mwili wa Kristo, tunaweza kuanguka kutoka katika neema, na kumwacha Bwana na njia yake, kama jinsi Mtume Paulo alivyo waonya Wagalatia.

Mtume Petro alisema kama tunataka kufanya mambo kama hayo, tunaweza kuzuia kuanguka kwetu.

2 Pet. 1:1-11, "*Simoni Petro, mtumwa na mtume wa Yesu Kristo, kwa wale waliopata imani pamoja na sisi yenye thamani katika hali ya Mungu wetu, na mwokozi Yesu Kristo. Neema na iwe kwenu na imani iongezwe katika kumjua Mungu na Yesu Bwana wetu. Kwa kuwa uweza wake wa Uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa, kwa kumjua yeye aliyetuita katika utukufu wake na wema wake mwenyewe. Tena kwa hayo ametukirimia ahadi kubwa mno, za thamani, ili kwamba kwa hizo mpate kuwa washirika wa tabia ya Uungu, mkiokolewa na uharibifu uliomo duniani kwa sababu ya tamaa. Naam, na kwa sababu iyo hiyo mkijitahidi sana kwa upande wenu, katika imani yenu tieni na wema, na katika wema wenu maarifa, na katika maarifa yenu kiasi, na katika kiasi chenu saburi, na katika saburi yenu utauwa, na katika utauwa wenu upendano wa ndugu, na katika upendano wa ndugu, upendo. Maana mambo hayo yakiwa kwenu na kujaa tele, yawafanya ninyi kuwa si wavivu wala si watu wasio na matunda, kwa kumjua Bwana wetu Yesu Kristo. Maana yeye asiyekuwa na hayo ni kipofu, hawezi kuona vitu vilivyo mbali, amesahau kule kutakaswa dhambi zake za zamani. Kwahiyo ndugu jitahidini kufanya imara kuitwa kwenu na uteule wenu; maana mkitenda hayo hamtajikwaa kamwe. Maana hivi mtaruzukiwa kwa ukarimu kuingia katika ufalme wa milele wa Bwana wetu, Mwokozi wetu Yesu Kristo.*"

Katika hili, ebu tuangalie mambo ambayo yanaweza kutufanya tusianguke.

Tegemea katika kile ambacho Mungu amekutendea

Mungu ametupatia vitu vyote.

Ahadi nyingi na kubwa tumehaidiwa ili kwamba tuwe washiriki wake wa uasili wake wa kipekee.

Kwa mipango yake tumeweza kukimbia machafuko ya dunia kupitia msamaha wake wa dhambi.

Mdo. 2:38, "*Petro akawaambia, tubuni, mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*"

Tumejaliwa kuwa wana wa Mungu.

1 Yohana 3:1, "*Tazameni ni pendo la namna gani alilotupa Baba, kwamba tuitwe wana wa Mungu; na ndivyo tulivyo. Kwa sababu hii ulimwengu haututambui, kwa kuwa haaukumtambui yeye.*"

Wana wa Mungu pia wamehaidiwa kuwa na Kristo kama wakili wao.

1 Yohana 2:1, "*Watoto wangu wadogo, nawaandikia haya ili kwamba msitende dhambi. Na kama mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki,*"

Watoto wake pia wamepewa ahadi nyingine ili kuwasaidia kumshinda Shetani wanapoanguka.

1 Kor. 10:13, "*Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu; ila Mungu ni mwaminifu ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo; lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlago wa kutokea, ili mweze kustahimili.*"

Kutafuta njia; imeahidiwa.

Tuna neno la Mungu linalotuongoza ili tujue anachotarajia kwetu.

Ameendelea mbele kwa undani zaidi ili aweze kutupa neno hilo.

Mdo. 20:32, "*Basi sasa nawaweka katika mikono ya Mungu, na kwa neno la neema yake ambalo laweza kuwajenga na kuwapa urithi pamoja nao waliotakaswa.*"

Roho Mtakatifu aliwaongoza mitume katika kweli yote.

Tunalo kanisa ambalo ndilo umoja wa ushirika katika kutupatia mazingira ya ukuaji kiroho.

Efe. 4:16, "*Katika yeye mwili wote ukiungamanishwa na kushikamanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadiri ya utendaji wa kila sehemu moja moja, huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo.*"

Tunayo damu ya Yesu ambayo huendelea kutusafisha na dhambi yote.

1 Yohana 1:7, "*Bali tukienenda nuruni kama yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi na damu yake Yesu Mwana wake, yatusafisha dhambi yote.*"

Kaa katika neno lake. Zab. 119:105, "*Neno lako ni taa ya miguu yangu, na mwangaza wa njia yangu.*"

Tunawezaje kukosa tukiwa na ahadi nzuri kama hizi? Ni nani atataka kuanguka kutoka katika ahadi hizi?

Weka malengo akilini

2 Pet. 1:4, "*Tupate na urithi usioharibika usio na uchafu, usionyauka, uliotunzwa mbinguni kwa ajili yenu.*"

Hilo ndio kusudi letu katika maisha. Lengo letu kuu ni kujitenga na uharibufu wa ulimwengu na kujichukulia asili ya kipekee ambao ndio tulioitiwa kuwa Wakristo.

Hatuwezi kukosa mtazamo wa malengo yetu. Shetani anataka kuweza vitu katika yetu na Mungu, na tunapaswa kuziondoa au kuachana nazo ili kwamba njia ya haki isifichwe kwetu.

Usijiweke katika hali ambayo Mungu hatakuwepo, na ambapo hutamwona Mungu.

Kuwa kiroho

2 Pet. 1:5-7, "*Naam, na kwa sababu iyo hiyo mkijitahidi sana kwa upande wenu, katika imani yenu tieni na wema, na katika wema wenu maarifa, na katika maarifa yenu kiasi, na katika kiasi chenu saburi, na katika saburi yenu utauwa, na katika utauwa wenu upendano wa ndugu, , na katika upendano wa ndugu, upendo.*"

Ujumbe huu unalenga kile ambacho kimeshasemwa kwa wakati mwingi kama wakati wa Wakristo.

Huu ndio mfumo wa ukuaji unao tarajiwa kwa kila Mkristo.

Mtu akiachaa kukua, anaanguka. Kuna nguvu katika ukuaji.

Ebu tutazame kwa karibu na tuone tunakua kwa kiasi:

Tunapaswa kukua katika fadhila.

Hii inatafsiria kama muunganiko wa uanadamu, nguvu, na nguvu kwa sababu ya wazo, hisia, na tendo la tabia njema. Usafi.

Fil. 4:8, "*Hatimaye ndugu zangu mambo yoyote yaliyo ya kweli, yoyote yaliyo ya staha, yoyote yaliyo ya haki, yoyote yaliyo safi, yoyote yenye kupendeza, yoyote yenye sifa njema; ukiwapo wema wowote, ikiwapo sifa nzuri yoyote, yatafakarini hayo.*"

Tunapaswa kukua katika hekima.

Hii huja kupitia kusoma na kujifunza neno la Mungu.

Kukataa hakuna udhuru. Mdo. 17:30, "*Basi zama zile za ujinga Mungu alijifanya kama hazioni; bali sasa anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu.*"

Kuwa na ujuzi wa neno la Mungu inatupatia kifaa kinachotufanya tusitende dhambi. Zaburi 119:11, "*Moyoni mwangu nimeliweka neno lako, nisije nikakutenda dhambi.*"

Tunapaswa kukua kwa kiasi.

Shetani anaweza kukutaka ufikirie kwamba hii inamanisha nini "fanya kwa utaratibu". Tenda dhambi kwa utaratibu? Mungu anakataa!

Hii inamanisha kuwa na kiasi.

Tumizi moja ni kuachana na kitu kinachoathiri.

Ni wazi kwamba wakati mtume Paulo alipomfundisha Feliki, moja ya mambo waliyoongelea ilikuwa ni utaratibu.

Mdo. 24:25, "*Na Paulo alipokuwa akitoa hoja zake katika habari za haki, na kuwa na kiasi, na hukumu itakayokuja, Feliki akafaanya hofu akajibu, sasa enenda zako nami nikipata nafasi nitakuita.*"

Tunapaswa kukua kwa subira.

Hii inamanisha uvumilivu or kusubiri

- Luka 21:19, "*Nanyi kwa subira yenu mtaziponya nafsi zenu.*"
- Yakobo 1:3-4, "*mkifahamu ya kuwa kujaribiwa kwa imani yenu huleta saburi. Saburi na iwe na kazi kamilifu, mpatekuwa wakamilifu na watimilifu bila kupungukiwa na neno.*"

Kama tungekuwa na uvumilivu wa Ayubu, tusingeshindwa.

Tunapaswa kukua katika uungu.

Zaidi kama Mungu tunakuwa wagumu kumwacha.

- 1 Tim. 4:7-8, "*Basi hadithi za kizee, zisizokuwa za dini uzikatae nawe <u>ujizoeze kupata utauwa</u>. Kwa maana kujizoeza kupata nguvu za mwili kwafaa kidogo, lakini utauwa hufaa kwa mambo yote; yaani unayo ahadi ya uzima wa sasa, nay a ule utakaokuwapo baadae.*"
- 1 Tim. 6:3-7, "*Mtu awaye yote akifundisha elimu nyingine, wala hayakubali maneno ya uzima, <u>wala mafundisho yapatanayo na utauwa</u>, amejivuna wala hafahamu neno lolote; bali anawazimu wa kuwazia habari za maswalia na mashindano ya maneno ambayo katika hayo hutoka husuda, na ugomvi, na matukano na shuku mbaya; na majadiliano ya watu walioharibika akili zao, walioikosa kweli huku wakidhani ya kuwa utauwa ni njia ya kupata faida. Walakini <u>utauwa pamoja na kuridhika ni faida kubwa</u>. Kwa maana hatukuja na kitu duniani, tena hatuwezi kutoka na kitu;*"

Tunapaswa kukuwa katika wema wa ndugu.

Wema wa ndugu ndio kitu ambacho wengi hukosa.

Wako tayari kwenda juu ya mtu anayekosesha, lakini badala yake, katika roho ya upole, mkaribie mtu huyo na umsaidie na mzigo wake.

Tunapaswa kukua katika wema, au upendo.

Hii ndio sehemu ya taji yetu ya ukuaji

- Rum. 12:9-10, "*Pendo na lisiwe na unafiki lichukieni lililo ovu, mkiambatana na lililo jemaa. Kwa pendo la undugu, mpendane ninyi kwa ninyi; kwa heshima mkiwatanguliza wenzenu.*"
- Rum. 13:10, "*Pendo halimfanyii jirani neno baya; basi pendo ndilo utimilifu wa sheria.*"

Tunapojifunza kupendaa kama Mungu alivyotupenda, basi tunakuwa kiroho.

Zaa matunda

2 Pet. 1:8, "*Maana mambo hayo yakiwa kwenu na kujaa tele, yawafanya ninyi kuwa si wavivu wala watu wasio na matunda, kwa kumjua Bwana wetu Yesu kristo.*

Tunapaswa kuzaa matunda maana tunaweza siyo tu kujua na kufanya mapenzi ya Mungu, bali tunaweza kufundisha pia, ya kuokoa nafsi, ya kumfanyia Bwana kazi, ya kulisaidia kanisa kukua.

Kama unazaa kama mwanafunzi, siyo kwamba hautaanguka.

Mkristo mvivu ambaye havutiwi katika kuokoa roho za watu ndiye yule anayekosaa furaha alafu anaanguka.

Kumbuka utakaso wako

2 Pet. 1:9, "*Maana yeye asiyekuwa na hayo ni kipofu, hawezi kuona vitu vilivyo mbali, amesahau kule kutakaswa dhambi zake za zamani.*"

Jifikirie mwenyewe unapotii injili ni kama kupata nguo mpya. Unapopata mavazi mapya, unakuwa makini ili zisichafuke. Ndio pale unaposahau mavazi mapya kwamba hauwi makini na kuziacha zichafuke.

Ndivyo ilivyo kwa maisha ya Mkristo. Tusisahau jinsi tulivyo wasafi tulipobatiza na kufanya tuwezalo kuwa mbali na dhambi.

Kuwa na juhudi

Tito 2:11-14, "*Maana neema ya Mungu iwaokoayo wanadamu wote imefunulia; nayo yatufundisha kukataa ubaya na tamaa za kudunia; tupate kuishi kwa kiasi na haki, na utauwa katika ulimwengu wa sasa; tukilitazamia tumaini lenye baraka na mafunuo na utukufu wa Kristo Yesu, Mungu mkuu na Mwokozi wetu; ambaye alijitoa nafsi yake kwa ajili yetu ili atukomboe na maasi yote, na kujisafishia watu wawe milki yake mwenyewe, wale walio na juhudi katika matendo mema.*"

Mungu alidhamiria watu wake wawe na juhudi katika matendo mema. Tunapaswa kuwa na juhudi, tufanye kazi kwa bidii, na kuwa macho.

Tukifanya haya hatutaanguka.